

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA**



MKUTANO WA TATU

YATOKANAYO NA KIKAO CHA KUMI NA TISA

13 MEI, 2016

MKUTANO WA TATU - YATOKANAYO NA KIKAO CHA KUMI NA TISA

TAREHE 13 MEI, 2016

I. DUA:

Saa 3.00 asubuhi Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) alisoma Dua na Kuongoza Bunge.

Makatibu Mezani

1. Ndg. Theonest Ruhilabake
2. Ndg. Zainab Issa

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani:-

1. Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi; Mhe. Hamad Yusuff Masauni aliwasilisha Mezani Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.
2. Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Nape Moses Nnauye aliwasilisha Mezani Hotuba ya Bajeti ya Wizara yake kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.
3. Mhe. Juma Selemani Nkambia aliwasilisha Mezani Taarifa ya Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka 2015/2016 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa 2016/2017.
4. Naibu Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Juu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Devota Minja aliwasilisha Taarifa ya Kambi juu ya Wizara hii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

III. MASWALI

Maswali yafuatayo yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge;

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

Swali Na.155 – Mhe. Kiteto Zawadi Koshuma

Swali la nyongeza: (i) Mhe.Kiteto Zawadi Koshuma

- (ii) Mhe. Suzan Anselm Lyimo
- (iii) Mhe. Edward Franz Mwalongo
- (iv) Mhe. Mary Pius Chatanda

Swali Na.156 – Mhe. Cosato David Chumi

- Swali la nyongeza: (i) Mhe. Cosato David Chumi
- (ii) Mhe. Edwin Mgante Sannda
 - (iii) Mhe. Mussa Ramadhani Sima
 - (iv) Mhe. Maryam Salum Msabaha

WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WAZEE NA WATOTO:

Swali Na.157 – Mhe. Ruth Hiyob Mollel

- Swali la nyongeza: (i) Mhe. Ruth Hiyob Mollel
- (ii) Mhe. Ritta Enespher Kabati

Swali Na.158 – Mhe. Mwantumu Dau Haji

Swali la nyongeza: Mhe. Mwantumu Dau Haji

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Swali Na.159 – Mhe. Mwitwa Mwikwabe Waitara

- Swali la nyongeza: (i) Mhe. Anthony Calist Komu [kny. Mhe. Hawa subira Mwaifunga]
- (ii) Mhe. Anthony Komu

WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:

Swali Na.160 – Mhe. Jacqueline Ngonyani Msongozi

Swali la nyongeza: (i) Mhe. Suleiman Masoud Nchambi

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

Swali Na.161 – Mhe. Elias John Kwandikwa

Swali la nyongeza: (i) Mhe. Elias John Kwandikwa

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

Swali Na.162 – Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki

Swali la nyongeza: (i) Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki

Swali Na. 163 – Mhe. Josephat Sinkamba Kandege

Nyongeza: Mhe, Josephat Sinkamba Kangege

WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

Swali Na.164 – Mhe. Abdallah Ally Mtolea

Swali la nyongeza: Mhe. Abdallah Ally Mtolea

IV. MATANGAZO:

- i. Wageni mbalimbali walioko kwenye *Galleries* walitangazwa.
- ii. Kikao cha Kamati ya Mitaji na Uwekezaji kitafanyika saa 7:00 mchana Hazina Ndogo.
- iii. Wabunge waende kupata huduma ya vitambulisho vya Taifa.
- iv. Katibu wa Wabunge Waislam anatangaza kwamba waislamu wajumuike pamoja kwa sala ya Al-Ijuma katika Msikiti wa Ghadafi.

Majibu ya Malalamiko (*Speaker's Rulling*):

Mhe. Naibu Spika alitoa majibu ya shutuma zilizotolewa na Mhe. Saed Kubenea dhidi ya Waziri wa Ulinzi Mhe. Dkt. Hussein Mwinyi na Jeshi la Ulinzi, Jeshi la Kujenga Taifa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Ambapo alimtaka pia Mhe. Saed Kubenea kutoa uthibitisho wa shutuma zake au afute shutuma hizo.

Mhe. Saed Kubenea alikataa kufuta kauli na hivyo kupewa siku nne ili aweze kuthibitisha shutuma zake kwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Susana Lyimo aliomba mwongozo kuhusu vitabu vya *contact* za Wabunge lini vitakuwa tayari?

V. HOJA ZA SERIKALI:

- Kwamba, Bunge sasa likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha, 2016/2017.
- Mhe. Juma Nkamia kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Mhe. Joseph Mbilinyi waliwasilisha Taarifa na Maoni yao juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

- Baada ya mawasilisho ya Mwakilishi wa Mwenyekiti wa Kamati na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Waheshimiwa Wabunge wafuatao walipata nafasi ya kuchangia hoja hii ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

1. Mhe. Mwitwa Mwikabe Waitara	-	CHADEMA
2. Mhe. Kabwe Zubeir Ruyagwa Zito	-	ACT
3. Mhe. Martha Moses Mlata	-	CCM
4. Mhe Agness Mathew Marwa	-	CCM
5. Mhe. Juma Selemani Nkamia	-	CCM

VI. KUSITISHA BUNGE:

Saa 6.55 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 10.00 jioni.

VII. BUNGE KUREJEA:

Saa 10.00 Bunge lilirejea na kuongozwa na Mwenyekiti, Mhe. Najma Murtaza Giga; Majadiliano yaliendelea kwa wafuatao walichangia Hoja ya Mhe. Waziri Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

6. Mhe. John Peter Kadutu	-	CCM
7. Mhe. Devotha Mathew Minja	-	CHADEMA
8. Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo	-	CCM
9. Mhe. Angelina Adam Malembeka	-	CCM
10. Mhe. Ahmed Juma Ngwali	-	CUF
11. Mhe. Venance Mwamtoto	-	CCM
12. Mhe. Amina Saleh Mollel	-	CCM
13. Mhe. Frank George Mwakajoka	-	CHADEMA
14. Mhe. Goodluck Asaph Mlinga	-	CCM
15. Mhe. Rashid Mussa Shangazi	-	CCM
16. Mhe. Hamidu Hassan Boobali	-	CUF
17. Mhe. Cosato David Chumi	-	CCM
18. Mhe. Maryam Salum Msabaha	-	CHADEMA
19. Mhe. January Makamba, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira		
20. Mhe. Harrison Mwakyemba Waziri wa Katiba na Sheria.		

KUFUTA KAULI:

Mhe. Angelina Malembeka aliomba nafasi akapewa na kufuta kauli yake ya kuudhi wakati anachangia Mjadala wa Habari ambapo alizungumzia masuala ya baadhi ya Waheshimiwa kupewa mimba na wengine kuwa na ndoa mbili.

MWONGOZO WA SPIKA:

- Mhe. Saed Ahmed Kubenea kwa kutumia Kanuni ya 68(7) na 64(1) (b) (f) na (g) alizungumzia kuhusu Mhe. Angelina Adam Malembeka kutoa lugha ya kuudhi wakati anachangia asiishie kufuta kauli bali athibitische kauli yake.
- Mhe. Suleiman Masoud Nchambi naye kwa kutumia Kanuni ya 68(7) na 64(1) (a) kwamba Mhe. Riziki Shahari Mngwali wakati anachangia alisema kwamba kuna mchezaji analipwa paundi elfu 32 ambazo ni karibu na milioni 300 kauli ambayo hana uhakika nayo na si ya kweli hivyo ni vyama wakati wa kuchangia mtu uwe na uhakika na unachosema.

Mhe. Mwenyekiti alitoa ahadi ya kujibu miongozo hiyo kwa wakati muafaka.

Baada ya miongozo hiyo Mhe. Naibu Waziri na Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo walijibu hoja za Waheshimiwa Wabunge.

VIII. KAMATI YA MATUMIZI:

Bunge liliingia katika hatua ya Kamati ya Bunge zima na kupitia Vifungu vya Wizara husika. Baada ya hapo Bunge lilirejea na mtoa hoja alitoa Taarifa na Bunge kuhojiwa na Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo ilipitishwa.

Tangazo:

- Kutakuwa na Semina kwa Wabunge wote kesho Jumamosi kuanzia saa 3.00 asubuhi

IX. KUAHIRISHA BUNGE:

Saa 2.30 Usiku Bunge liliahirishwa hadi tarehe 16/5/2016 siku ya Jumatatu saa 3.00 asubuhi.

**DODOMA
13 MEI, 2015**

**DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE**